

Watetezi kutoka Office of the Education Ombuds ya Gavana wa Jimbo la Washington: Mpango wa Mikakati

(Agosti 2020-2023)



Vipaumbele vya Mikakati

Utatuzi wa Migogoro Usio Rasmi

Office of the Education Ombuds (OEO) humsaidia mtu yeyote aliye na maswali au hoja kuhusu shule za umma za K-12 za Washington. Tunaweza kukupa maelezo, rufaa, zana na rasilimali nyingine.

Madhumuni ya kisheria ya Office of the Education Ombuds (OEO) ni kupunguza ukosefu wa fursa. Vipaumbele vya mpango wetu wa mikakati hulenga haki ya elimu, hasa kwa jamii zilizoathiriwa sana na COVID-19. Tunatumia rasilimali zetu ndogo za utatuzi wa migogoro, kama vile upatanishi na ukufunzi usio rasmi, kwa [wanafunzi wa K-12 ambao](#):

- Hawapo shuleni, ikijumuisha wanafunzi wenye ulemavu wanaopokea huduma ya baadhi ya siku za shule
- Ni watu wa asili ya Kiafrika au wa makabila asili
- Hawana makao
- Wanatunzwa na jamaa au vituo vya makazi
- Wanashiriki katika masuala ya haki kwa vijana au mifumo ya kuwarekebisha vijana
- Ni wahamiaji rasmi au wasio rasmi, wakimbizi, watafutaji makazi rasmi au wanafunzi au familia ambazo lugha yao msingi si Kiingereza au
- Wanapokea usaidizi wa Mipango ya Wraparound yenye Huduma za Kina (Wraparound with Intensive Services, WISE) au Mipango ya Wagonjwa Wanaolazwa ya Muda Mrefu kwa Watoto (Children's Long Term Inpatient Programs)

Mikakati:

Kujenga mahusiano na familia, wanafunzi na jamii zinazotafuta haki ya elimu katika shule na kusikiliza na kufahamu nguvu zao na mambo waliyopitia

Kuunda zana zaidi za mtandaoni za kujibu maswali yanayoulizwa sana yaliyo nje ya vipaumbele vya ukabilianaji wa moja kwa moja

Kutambua fursa za kusababisha mabadiliko ya kimfumo kupitia hoja za watu binafsi zilizowasilishwa kwetu

Huduma kwa jamii

Vipaumbele vyetu vya huduma kwa jamii vinaonyesha jamii zilizopewa kipaumbele kwenye juhudi zetu za kutatua migogoro. Pia tutatengeneza nyenzo na zana za masuala nje ya mpango wetu wa kimbakati wa kuwezesha familia, wanafunzi, na waelimishaji kushirikiana.

Mikakati:

Kushirikiana na mashirika ya jamii, familia, wanafunzi na waelimishaji, na pia mashirika ya serikali kuandaa hafla na semina

Kuimarisha mahusiano yanayoendelea na mashirika na vikundi vya familia na wanafunzi, huku pia tukiongeza uhamasisho kuhusu Office of the Education Ombuds (OEO) katika jimbo lote

Kutumia mbinu bora ya kusimulia matukio ya familia na wanafunzi kwa waelimishaji, watunga sera na familia na jamii nyingine

Utetezi wa Sera

Tutatambua na kutoa fursa za kutoa hamasisho kuhusu haki dhidi ya ubaguzi wa rangi, ulemavu na afya ya kiakili, na ufikiaji wa lugha katika mfumo wa elimu. Tutajumuisha mitazamo na hoja za wanafunzi, familia, na jamii katika majadiliano na maamuzi ya sera.

Mikakati:

Kushirikiana na mashirika ya jamii, familia, na wanafunzi kupambana na ubaguzi wa rangi, kiuwezo, na aina nyingine za ukandamizaji

Kujifunza kutokana na, na kuongozwa na mitazamo jamii, familia, na wanafunzi ambayo mara nyingi hupuzwa wakati wa kutunga sera

Kutumia majukumu yetu ya uongozi kwa jopokazi kutetea maoni ya familia na wanafunzi

MAONO: Maono yetu ni kuwa na mfumo wa elimu ya umma unaoondoa ubaguzi wa rangi, kiuwezo na ubaguzi mwingine ili kumwezesha kila mwanafunzi kutimiza ndoto zake za siku zijazo.

Tunathamini uhuru wetu, maadili ya kukabiliana na ubaguzi wa rangi, na kuwajibikia jamii. Tutajifunza kama timu kutoka kwa familia, wanafunzi, na jamii na kukuza maono haya.

MADHUMUNI

Tunashirikiana na familia, jamii, na shule kushughulikia matatizo kwa pamoja ili kila mwanafunzi aweze kushiriki kikamilifu na kufanikiwa katika shule za umma za K-12 za Washington.

MAJUKUMU YETU

Kusikiliza na ushughulikia maswali juu ya mfumo wa elimu ya umma wa K-12

Kutumia mbinu za utatuzi wa migogoro zisizo rasmi ili kuwezesha suluhisho za kushirikiana na kukuza haki ya kielimu

Kutoa ukufunzi, uwezeshashi na mafunzo kuhusu ushiriki wa familia na jamii na utetezi wa kimifumo

Kukusanya data na kutambua mabadiliko yatakayotuwzesha kutoa mapendekezo ya sera ya elimu

